
# MEMORANDUM OF UNDERSTANDING

- SUGAR PLANT OF 5000 TCD ALONG WITH CO-GEN UNIT AND FERTILIZER PLANT
- DISTILLERY (ETHANOL) PLANT WITH
- ZERO POLLUTION EFFLUENT TREATMENT PLANT



## GREEN POWER PROJECT











**MEMORANDUM OF UNDERSTANDING**
**BETWEEN**
**NKUSU THEO SUGAR LIMITED AND**
**NAKAWALE VILLAGE – SONGEA DC**


NTS Nkusu Theo Sugar

Corporate Office:
1392 New Forest, Block M, Regional Hospital Road, P.O. Box 2406, Mbeya – Tanzania
Website: www.nkusutheosugar.com
U.S.Office:
8276 Humphrey Ln., Manassas VA 20109 United States of America


**AND**

## NAKAWALE VILLAGE – SONGEA DC


P.O. BOX 995 SONGEA DC – With a permanent office located in Nakawale village, Peramiho at Songea District in Ruvuma Region - Tanzania

# MKATABA WA MAKUBALIANO

## KATI YA

## HALMASHAURI YA KIJIJI CHA NAKAWALE NA KAMPUNI YA NKUSU THEO SUGAR LIMITED

Mkataba huu wa makubaliano umefanyika leo hii 29 Siku ya 09 2018.

Katika huu mkataba wa makubaliano, Halmashauri ya Kijiji cha **Nakawale**, ni moja ya vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kilichoanzishwa kwa mujibu wa sheria, kwasababu ya Mkataba huu anuani yake ni; S.L.P. 995 Songea – kwa anwani ya kudumu yenye ofisi zilizopo Kijijini Nakawale, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mkoani Ruvuma – Tanzania, kwa upande mmoja.

**NA**

**Nkusu Theo Sugar Limited,** ni kampuni binafsi, iliyosajiliwa Mei 18, 2013, katika sheria ya uanzishwaji wa makampuni ya mwaka 2002 ibara 15, yenye makao yake makuu kitalu 1392 New Forest, Block M, Region Hospital Road, S.L.P 2406, Mbeya - Tanzania, namba ya simu +255 (0) 755 107907, 255 (0) 754 275416 pamoja na ofisi iliyoko Marekani, kitalu 8276 Humphrey Ln, Manassas, Virginia 20109, United States of America, namba ya simu +1 (703) 828-7354, kwa upande mwingine.

### 1. TAFSIRI

Katika mkataba huu , vifupisho vya baadhi ya maneno yalitomukia na maana yake kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **MM** | Mkataba wa Makubaliano |
| **Pande** | Nakawale Village Council na Nkusu Theo Sugar Limited |
| **KLPD** | Kilolita kwa siku |
| **TCD** | Kusagwa Tani kwa Siku |

**Mwekezaji** Nkusu Theo Sugar Limited

## 2. DHUMUNI LA MKATABA HUU WA MAKUBALIANO

Dhumuni la Mkataba huu ni kuleta uhusiano wa ubia baina ya Halmashauri ya Kijiji cha Nakawale na Kampuni ya Nkusu Theo Sugar Limited .

## UWIANO WA MRADI

### 3.1 Uletaji wa ajira

Mradi huu unategemewa kutengeneza ajira ya wafanyakazi zisizopungua elfu ishirini (20,000/=) hii ni pamoja na ajira za kutwa na za kudumu.

### 3.2 Wazalishaji wa nje.

Katika kipindi chote cha uwekezaji, Wanakijiji wanaozunguka eneo la mradi watakuwa na fursa ya kulima miwa na kuuza kwa Mwekezaji moja kwa moja. Kwa upande mwingine kutakuwa na uboreshaji wa ugani katika makundi yote yatakayoundwa na kushiriki katika ulimaji wa miwa. Kutakuwa na soko la uhakika kwa bidhaa zao za miwa, mafunzo, pamoja na kuunganishwa na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya riba nafuu.

### 3.3 MAJUKUMU YA KAMPUNI KATIKA JAMII.

Mwekezaji anategemea kuanza ujenzi Kituo cha Afya cha Nakawale kuanzia Januari 2019 mpaka Disemba 2019. Mwekezaji baada ya kuanza uzalishaji hapo baadae atajenga shule na kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Baadhi ya miradi itakayotekelezwa na mwekezaji baada ya kuanza kwa uzalishaji baada ya kupata gawiwo ni :

- Ujenzi wa shule ya Sekondari kwa viwango vinavyokubalika kwa serikali na kutoa elimu bure kwa Wanakijiji.
- Mradi wa maji safi, utajengwa na mwekezaji kwa ajili ya shughuli za kiwanda na matumizi ya kijiji kwa ujumla..

- Uanzishaji na utekelezaji wa shughuli za Michezo mbalimbali kwa wafanyakazi pamoja na wanakijiji wanaouzunguka mradi.

- Kutengeneza asilimia 90 % ya ajira zisizokuwa za utaalamu na kuhakikisha ni fursa kwa Wazawa wa Nakawale.

- Kampuni kwa kushirikiana na mzazi husika itafadhili masomo ya elimu ya juu, pale itakapothibitisha kuwa familia ya mwanafunzi husika kutokuwa na uwezo wa kugharamia elimu ya juu ndani ya Tanzania.

## 4. MPANGO WA USHIRIKIANO

### 4.1 Kwa ujumla

4.1.1 Halmashauri ya Kijiji cha Nakawale inamkaribisha Mwekezaji Nkusu Theo Sugar Limited kuzalisha sukari, umeme, ethanol na mbolea kijijini Nakawale, Songea, Ruvuma –Tanzania. Kuuza kwa kuziba pengo ndani ya nchi pamoja na kuuza nje ya nchi.

4.1.2 Mradi huu utafanyika katika Kijiji cha Nakawale katika kata ya Muhukulu.

*4.1.3* Kijiji kitapata asilimia 3 % ya hisa za umiliki wa kampuni, zitakazowezesha kijiji kupata gawiwo litakalotokana na umiliki huo.

### 4.2 MAJUKUMU YA KILA PANDE

**4.2.1 Halmashauri ya Kijiji cha Nakawale**

4.2.1.1 Halmashauri ya Kijiji cha Nakawale, ni kuhakikisha Ardhi ya uwezaji inapatikana, ambapo ardhi yenye ukubwa wa ekari 35,398 kwa ajili ya mwekezaji imepatikana baada ya upimaji wa awali uliofanyika mwezi machi 2018.

**4.2.2 Nkusu Theo Sugar Limited**

4.2.2.1 Mradi wote ulioelezwa unahitaji hekari elfu hamsini (50,000) kwa awamu mbili za utekelezaji. Nkusu Theo Sugar Limited kwa upande wake watakamilisha yote yanayohitajika ili kuwezesha uzalishaji kamili wa sukari tani 5,000 TCD kwa siku, umeme 23.5 MW, Ethanol 60 KLPD na Mbolea tani 20,000. Nkusu Theo Sugar Limited, itajenga mtambo maalum wa kuondoa uchafuzi wa maji na mazingira (Zero Pollution Effluent Plant), uendelezaji wa miwa, majengo na Teknolojia.

4.2.2.2 Mwekezaji amechangia kiasi cha shilingi milioni kumi na tano (15,000,000/=) kwa Halmashuari ya Wilaya ya Songea kwa ajili ya shughuli za upimaji wa awali na kuhuisha mpango wa matumizi bora ya ardhi kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Songea kutokuwa na bajeti ya kufanya shughuli hizo kwa wakati huo.

## 5. AHADI YA UBIA

4.3 **Hivyo,** Mkataba huu wa Makubaliano utatumika rasmi baada ya kusainiwa na pande husika, na utadumu kwa muda wa miaka mitano (5). Uhuishaji wa Mkataba huu utafanywa kwa mazungumzo ya pande husika.

4.4 **Hivyo,** Mkataba huu wa Makubaliano unasimiwa na sheria za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

4.5 **Hivyo**. Endapo kutatokea na tofauti baina ya Pande husika, tofauti hizo zitamalizwa kwa njia ya mazungumzo na endapo itashindikana suala hilo litawasilishwa Mahakamani kwa utatuzi.

## 6. DHAMANA

Pande zote mbili (Halmashauri ya Kijiji cha Nakawalel na Nkusu Theo Sugar Limited) wana dhamana kisheria ya kubeba majukumu yote yaliyo kwenye Mkataba huu wa Makubaliano.

**UMESAINIWA SONGEA NA KUWEKWA MUHURI WA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA NAKAWALE**

Leo 29 siku ya 09 2018

MUHURI

HALMASHAURI YA KIJIJI ... NAKAWALE SONGEA
MWENYEKITI ... 29/09/2018

MBELE YANGU:

Jina: ALLY SEIFU NASWERE
Anwani: S.L.P 995 SONGEA
Saini: [signature]
Cheo: MWENYEKITI WA KIJIJI

Jina: COSMAS ELIAS MBULE
Anwani: S.L.P 995 SONGEA
Saini: [signature]
CHEO: AFISA MTENDAJI WA KIJIJI

Nkusu Theo Sugar LTD
8276 Humphrey Ln
Manassas, VA 20109
United States of America

**UMESAINIWA SONGEA NA KUWEKWA MUHURI WA KAMPUNI YA NKUSU THEO SUGAR LIMITED**

Leo 29 siku ya 09 2018

MUHURI

**MBELE YANGU:**

Jina LONGINUS D. KAGARUKI
Anwani S.L.P. 2406, MBEYA
Saini [signature]
Cheo MKURUGENZI WA FEDHA NA UTAWALA

Jina [illegible] T. [illegible]
Anwani S.L.P. 2406, MBEYA
Saini [signature]
Cheo MKURUGENZI WA SHUGHULI

TANGANYIKA
REGISTRY OF DOCUMENTS

Presented 20-2-2019 at 01:30 Pm.
Registered as Folio No. 3734-MBYOR
No. 322/2019 in the General Register
Fee Shs. 8000/= paid vide Receipt No. 990129310019.

Asst. Registrar of Documents

TANGANYIKA STAMP DUTY ACT
Stamp Duty Shs: 500/= Paid
and Revenue Receipt No. 990129310019.
of 20-2-2019. Issued.

Stamp Duty Officer

TANGANYIKA STAMP DUTY ACT
Stamp Duty Shs: 1000/= Paid
on original Receipt No. 990129310019.
of 20-2-2019.

Stamp Duty Officer